**RAUDHWA MODERN ISLAMIC SECONDARY SCHOOL**

P.O.BOX 166,
NYAKANAZI - BIHARAMULO - KAGERA
RAUDHWA SCHOOLS

PHONE :+255789 588 152
+255758259520
+255715712238
EMAIL : raudhwaschools@gmail.com

# FOMU YA MAOMBI YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA TANO 2026/2027

*(Sehemu zote zilizo wazi zijazwe kwa herufi kubwa)*

**Picha ya mwanafunzi ya hivi karibuni**

## 1. TAARIFA ZA MUOMBAJI

A. Jina la Mwanafunzi ……………………………………………………………

- Kwa mwanafunzi anayejiunga na kidato cha tano au cha sita, andika majina uliyotumia katika mtihani wa kumaliza elimu ya kidato cha nne (NECTA).

B. Tarehe ya kuzaliwa ……………………………………………………….....................

C. Mahali alipozaliwa

Mkoa ……………...………. Wilaya …………………………… Kata …………………….

D. Uraia ………………………………………………………………………………...

E. Dini …………………………………………… Dhehebu ……………………………………

## 2. TAARIFA ZA MZAZI/ MLEZI

A. Jina la Mzazi/Mlezi ……………………………………………………………………………

B. Anwani kamili

Mkoa ……………...………. Wilaya …………………………… kata ……………………

C. Namba ya simu ya mkononi ………………………………………………

D. Namba ya simu (i) Kazini ……………….……………….

(ii) Nyumbani ………….………..………

E. Kazi ya Mzazi/Mlezi ……………………………………………………….......................

☐ ***Kumbuka kuandika namba ya simu na anwani kamili, ni muhimu sana.***

## MATOKEO YA MTIHANI WA TAIFA YA KIDATO CHA NNE

| Mwaka Wa Kuhitimu | Namba Ya Mtihani | Daraja | Pointi |
|---|---|---|---|
| | | | |

## 3. ORODHA YA TAHASUSI ZINAZOPATIKANA SHULENI

| Sayansi | Weka √ | Sanaa | Weka √ | Biashara | Weka √ | DINI | Weka √ |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| PCB | | HKL | | EGM | | IHG | |
| PCM | | HGK | | ECA | | IHL | |
| CBG | | HGL | | HGE | | IHK | |
| PGM | | KLAr | | | | IHAr | |

## 4. SIFA BINAFSI ZA KUJIUNGA

Mwanafunzi anayejiunga na shule hii kidato cha tano au sita anapaswa kuwa na vigezo vya jumla kama vilivyoainishwa na Baraza la Mitihani la Tanzania chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kama ifuatavyo:

i. Ufaulu wa **daraja la kwanza** kwa tahasusi za Sanaa, biashara na dini.
ii. Ufaulu wa **daraja la kwanza hadi la pili** kwa tahasusi za sayansi.

## 5. TAARIFA ZA SHULE ANAYOTOKA MWANAFUNZI (kwa wanaohamia)

A. Jina la shule anayotoka ………………………………………………………………………….

B. Mwaka aliopokelewa kwenye hiyo shule aliyotoka ……………………………………………….

C. Kidato na tahasusi aliyokuwa anasoma kwenye shule aliyotoka ………………..

D. Kidato na tahasusi anayoomba kujiunga nayo shuleni hapa ………………….

E. Namba ya mtihani ya kumaliza Elimu ya kidato cha nne ……………………………….

## 6. KUHUSU FOMU HII

Fomu hii ijazwe na kuletwa shuleni Raudhwa Modern Islamic kabla au ifikapo tarehe 30 Juni 2026.

Saini ya Mzazi/Mlezi ………………………………….. Tarehe ………………..………………

## 7. KWA MWANAFUNZI

Ninaahidi kufuata na kutii sheria zote za shule endapo nitachaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari Raudhwa Modern Islamic.

Saini ya Mwanafunzi …………………………………….…  Tarehe …………………………

***MUHIMU***

***a)*** Shule yetu inapokea mwanafunzi wa **BWENI TU**.
***b)*** Fomu hii itachangiwa **Tsh 20,000/= (elfu ishirini tu)** itakayokabidhiwa kwa aliyekupatia fomu hii. (**fomu iwe imesainiwa na kuwekwa muhuli wa ofisi**)

**MKURUGENZI WA SHULE**

**MAWASILIANO:**

**Mkuu wa shule – 0768688341 au 0760887204**

**Meneja wa Shule – 0768688341 au 0756982224**

**Mkurugenzi wa Shule – 0767812235**

RAUDHWA MODERN ISLAMIC SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 166,
NYAKANAZI - BIHARAMULO - KAGERA
RAUDHWA SCHOOLS
PHONE :+255789 588 152
+255758259520
+255715712238
EMAIL : raudhwaschools@gmail.com

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO – 2026/2027

## 1. UTANGULIZI

Tunayo furaha kukuarifu kuwa mwanao ………………………………………………………… amechaguliwa kujiunga na shule ya **Sekondari Raudhwa Modern Islamic** iliyopo wilaya ya **Biharamulo** Mkoa wa **Kagera**. Mwanao anatakiwa kuripoti shule tarehe **4 Julai, 2026.**

Shule ya Sekondari Raudhwa Modern Islamic inafundisha masomo ya **Sayansi, Sanaa, Biashara na dini**. Mwanafunzi anapojiunga hana budi kuyasoma kwa bidii masomo aliyochaguliwa na kufaulu kwa kiwango cha juu.

Tafadhali hakikisha mwanao anaripoti siku iliyopangwa. Hatupokei mwanafunzi **usiku** mzazi akipata dharura atoe taarifa mapema shuleni**.** Masomo yataanza mara moja baada ya kufungua shule. Mwanafunzi awapo shuleni anapaswa kuutumia muda wake ipasavyo katika masomo na si vinginevyo.

## 2. MALIPO YA KUJIUNGA NA SHULE

### A. ADA YA SHULE NA MICHANGO

**i.** Ada ya shule ni Sh. 2**,000,000/= (Milioni mbili)** kwa mwaka.

✓ Inaruhusiwa kulipa ada kwa awamu moja mpaka nne katika mchanganuo ufuatao:

| Awamu ya Kwanza | Awamu ya Pili | Awamu ya Tatu | Awamu ya Nne |
|---|---|---|---|
| *30 Juni , 2026* | *30 Septembai, 2026* | *30 Disemba, 2026* | *30 Machi, 2027* |
| Sh. 700,000/= | Sh. 500,000/= | Sh. 400,000/= | Sh. 400,000/= |

**ii. Michango mingine (Michango yote inalipwa mwanzoni).**

| Aina Ya Mchango | Mahafari | | Mitihani Kidato Cha Sita | Futari |
|---|---|---|---|---|
| | Kidato Cha Tano | Kidato Cha Sita | | |
| Kiasi | **50,000/=** | **100,000/=** | **150,000/=** | **60,000/=** |

**iii. Malipo ya Sare za shule ni**

a) **300,000/= kwa Wasichana**

**b) 450,000/= kwa Wavulana**

## MALIPO YOTE YAPITIE BENKI TU KATIKA AKAUNTI ZIFUATAZO.

Bank: **NMB**
A/c Number: **51510043318**
A/c Name: **RAUDHWA MODERN ISLAMIC SCHOOL**

Benki: **TCB (BENKI YA POSTA)**
Namba ya Akaunti: **251405000014**
Jina la Akaunti: **RAUDHWA MODERN ISLAMIC**

**AU**

Benki: **CRDB**
Namba ya Akaunti: **0150001J01B00**
Jina la Akaunti: **RAUDHWA MODERN ISLAMIC**

**ZINGATIA:**

i. Shule haipokei fedha taslimu.
ii. Malipo ya sare na michango yote yanalipwa mara moja kwa mkupuo kabla ya mtoto kuripoti shuleni.
iii. Mwanafunzi ambaye hajakamilisha malipo hapokelewi shuleni.

## 3. MAHITAJI MENGINE AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO:

- **Mahitaji ya usajili**

i. Picha 4 za passport size za mwanafunzi za hivi karibuni.
ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
iii. Nakala ya cheti au hati ya matokeo ya mtihani wa kuhitimu kidato cha nne.
iv. Jalada (spring file) moja kwa ajili kuhifadhia kumbukumbu za mwanafunzi.
v. Rimu 2 (Aina ya **Double A tu**). Inasisitizwa kuwa isinunuliwe aina tofauti na iliyoagizwa.

- **Mahitaji ya Darasani**

| Na | Kifaa | Idadi |
|---|---|---|
| 1 | Begi la kutunzia madaftari | 1 |
| 2 | Daftari counter book (Quire 3) | 12 |
| 3 | Daftari ndogo za mazoezi (msomi) | 24 |
| 4 | Kalamu za wino | 25 |
| 5 | Majaradio | 12 |
| 6 | Mkebe wa hesabu | 1 |
| 7 | Penseli (HB) | Dazeni 1 |
| 8 | Rula | 2 |
| 9 | Scientific Calculator (PCM, PCB, PGM, CBG, EGM na HGE) | 1 |
| 10 | Jalada (Box file) kwa ajili ya kuhifadhia mitihani na majaribio | 1 |

- **Mahitaji ya Bweni na usafi binafsi**

| Na | Kifaa | Idadi |
|---|---|---|
| 1. | Godoro aina ya **DODOMA/SUPER BANCO** (upana inch 4 na urefu wa futi 2.5/6) | 1 |
| 2. | Shuka rangi ya pinki | 2 |
| 3. | Shuka rangi ya bluu | 2 |
| 4. | Blanketi | 1 |
| 5. | Chandarua rangi nyeupe | 1 |
| 6. | Sanduku la chuma (Trunk) kubwa lenye kufuli 2 | 1 |
| 7. | Dawa ya meno kubwa Gramu 250 | 2 |
| 8. | Miswaki | 4 |
| 9. | Dodoki la kuogea la kuvaa kiganjani | 2 |
| 10. | Sabuni za kuogea (medicated soap) | Dazeni 1 |
| 11. | Sabuni ya unga kwa muhula mzima | Kilo 6 |
| 12. | Sabuni za mche (white wash, Jamaa, Family au Mukwano) kwa muhula mzima | 5 |
| 13. | Rangi ya kung'arisha viatu ya mkebe (Gramu 80) | 2 |
| 14. | Brashi za kung'arishia viatu | 2 |
| 15. | Brashi za kuoshea viatu | 2 |
| 16. | Mafuta ya kupaka (mgando) Gramu 500 | 2 |
| 17. | Kata kucha | 2 |
| 18. | Beseni | 1 |
| 19. | Ndoo ndogo | 1 |
| 20. | Kopo la kuogea | 1 |
| 21. | Taulo | 1 |
| 22. | Yebo za kuogea | Pea 1 |
| 23. | Kitana | 1 |
| 24. | Nguo za kulalia | Pea 2 |
| 25. | Kanzu rangi nyeupe kwa wavulana (aje akiwa amevaa) | 2 |
| 26. | Baibui na juba rangi nyeusi isiyo na urembo kwa wasichana (aje akiwa amevaa) | 2 |
| 27. | Boxer kwa wanafunzi wa kiume | Zisizopungua 6 |
| 28. | Chupi/taiti kwa wanafunzi wa kike | Zisizopungua 10 |
| 29. | Vest/Kaushi | Zisizopungua 6 |
| 30. | Mkanda wa kuvalia suruali wa Ngozi | 1 |
| 31. | Viatu vya wazi (open shoes) si yeboyebo | Pea 1 |
| 32. | Viatu vya Ngozi rangi nyeusi (visiwe na visigino virefu na si buti) | Pea 2 |
| 33. | Viatu vya michezo (raba) rangi nyeupe | Pea 1 |
| 34. | Soksi rangi nyeusi | Pea 6 |
| 35. | Kitenge kwa wasichana | Pea 1 |
| 36. | Vyombo vya chakula (kikombe cha mfupa na Sahani ya bati yenye patisheni) | 1 |
| 37. | Taulo za kike kwa wasichana | Za kutosha |

***MUHIMU:***

Ili kuepuka upotevu, vifaa vyote vya mwanafunzi viandikwe majina kamili ya mwanafunzi ikiwa ni pamoja na nguo zake zote kwa kutumia rangi maalumu ya ku-print maandishi kwenye nguo na siyo *Correction Fluid*.

**KUMBUKA:**

Shule haitampokea mwanafunzi mwenye mapungufu ya vifaa au vifaa ambavyo havijaandikwa majina kamili ya mwanafunzi husika.

## 4. KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini, hivyo unatakiwa kuzingatia utaratibu, kanuni na sheria za shule ili shule iweze kuendesha shughuli zake za kila siku bila matatizo. Kanuni na taratibu za shule zinalenga kumpa mwanafunzi **UTII**, **HESHIMA** na **NIDHAMU** katika kusoma kwake.

1. Lugha ya mawasiliano ni Kiingereza.
2. Mwanafunzi ni lazima kuwahi shuleni pindi shule inapofunguliwa.
3. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare za shule wakati wote wa shughuli za kishule ndani na nje ya shule.
4. Mwanafunzi ni lazima kuletwa na kufuatwa shuleni na mzazi/mlezi aliyeandikishwa shuleni katika siku, tarehe na muda uliopangwa akiwa amevaa sare ya shule iliyokamilika. Iwapo atachelewa kufika katika tarehe na muda uliopangwa hatapokelewa.
5. Ni lazima mwanafunzi kupimwa na kuleta **Medical Form** iliyojazwa na daktari kila ajapo shuleni baada ya likizo. Pia mwanafunzi mwenye matatizo ya kiafya lazima aufahamishe uongozi wa shule mara afikapo shuleni. Mwanafunzi haruhusiwi kutunza dawa yoyote bwenini. Dawa zote zitapokelewa na kutunzwa kwa mtoa huduma ya kwanza wa shule au mlezi anayehusika. Endapo mwanafunzi ana kadi ya bima ya afya anashauriwa kuja nayo na kuikabidhi kwa uongozi wa shule.
6. Mwanafunzi haruhusiwi kuja shuleni na simu, nguo za nyumbani, vipodozi, vyakula, madawa ya kulevya au kilevi (pombe) ya aina yoyote na kuvitumia, heleni, pete, bangili, perfume, radio, TV, ipad (na vifaa vingine vya kielectroniki), n.k.
7. Mwanafunzi haruhusiwi kuendesha gari, pikipiki, au bajaji ndani ya eneo la shule.
8. Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kutoka/kutoroka kwenda nje ya shule aidha kwa kuruka uzio wa shule au kwa namna nyingine yoyote na kama ni muhimu shule itampeleka na kumrudisha.
   Mfano: Hospitali na siyo sokoni wala madukani.
9. Mwanafunzi harushusiwi kutembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum: staffroom (ofisi za walimu), ofisi za shule, maabara, jikoni, na nyumba za walimu na wafanyakazi wasio waalimu.
10. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria bila kukosa shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika kalenda ya shule, ratiba ya muongozo wa shughuli za kitaaluma (School Academic Schedule) na ratiba ya kila siku (School Daily Routine).

11. Ni marufuku kwa mwanafunzi kupiga kelele darasani, maktaba, maabara, mabwenini, paredi n.k. pamoja na kugoma, kuchochea au kuongoza mgomo au vurugu/ugomvi utakaosababisha kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni. Hivyo ni marufuku kwa mwanafunzi kupigana au kumpiga mwanafunzi mwenzake au mtumishi.

12. Ni marufuku mwanafunzi yeyote kujihusisha au kushiriki katika vitendo vya wizi wa namna yoyote awapo shuleni na anatakiwa kutunza mali za shule na vifaa vyake binafsi. Endapo atasababisha upotevu, au uharibifu wa aina yoyote ile wa mali za shule atatakiwa kulipa au kuleta mali hizo. Mfano; vitabu, n.k.
13. Mwanafunzi anapaswa kunyoa nywele katika namna ambayo nywele zake zote kichwani zilingane na ziwe fupi za kutumia kitana kidogo. Unyoaji usiofaa ambao ni pamoja na unyoaji wa panki, denge na mitindo mingine yoyote inayofanana na hiyo, hairuhusiwi kwa mwanafunzi yeyote awapo shuleni.

14. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kufanya usafi wa mazingira pamoja na usafi wake binafsi na kutandika kitanda. Ni kosa kwa mwanafunzi kutupa taka maeneo yasiyo rasmi au kuziona takataka bila kuziondoa, hii ni pamoja na kumwaga taka zilizomo kwenye vyombo vya kutunzia taka kwa muda (dustbins) kwa ajili ya kutunza mazingira ya shule. Ni marufuku kuchora picha kuandika maandishi katika dawati, meza, viti, vitanda, vitabu au kwenye kuta za majengo ya shule n.k. Ili kudumisha afya njema mwanafunzi hapaswi kuchangia vyombo vya chakula na mwenzie wala kula kwenye kundi, asitupe ovyo mabaki ya chakula wala kutunza chakula muda usio rasmi kwa chakula, asifuge nywele ndefu, kucha, ndevu, asipake kucha rangi.

15. Ni kosa kwa mwanafunzi kupita katika eneo lisilo na barabara maalumu ikiwa ni pamoja na kupitia madirishani.

16. Mwanafunzi ni lazima awe na heshima, adabu na utii katika nyanja zote. Asigomee au kukataa adhabu halali. Asitumie lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu na kwa watu wengine, asimame mwalimu, wafanyakazi wasio waalimu, mzazi au mlezi, mgeni au mtu anayemzidi umri anapopita, anapoingia darasani na kwenye ukumbi wa mikutano. Awaheshimu wafanyakazi wote waliopo shuleni kama walezi wake. Asivae mikanda mipana au yenye bakoli kubwa na isiwe na urembo (picha), suruali za mitindo kama vile modo na kuvaa mlegezo (sketi au suruali), kwahiyo mwanafunzi anatakiwa kuwa na nidhamu wakati wote awapo shuleni na nyumbani.

17. Ni kosa mwanafunzi kumdharau kiranja au viranja wa shule kwani kufanya hivyo ni kuwadharau walimu waliomkabidhi madaraka, hii ni kwa sababu viranja wanafanya kazi kwa niaba ya walimu na wanafunzi wote. Viranja wote waliochaguliwa hapa shuleni ni viranja wa shule nzima na wanayo madaraka kamili juu ya kila mwanafunzi bila kujali ni wa darasa gani au eneo gani. Heshima na utii ni vya lazima.
18. Ni kosa kwa wanafunzi kulala wawili au zaidi katika kitanda kimoja. Endapo mwanafunzi atabainika kufanya hivyo hatua kali za kinidhamu zitachuliwa dhidi yake, hii ni pamoja na kusimamishwa masomo.

19. Ni marufuku kwa mwanafunzi kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi au kukutwa kitu chochote kinachohusiana na mapenzi, mfano; barua, kadi, daftari la nyimbo za mapenzi na miziki, picha, n.k.

20. Mwanafunzi awapo hapa shuleni, ataendelea kuabudu katika dini/dhehebu la imani yake aliyotoka nayo nyumbani na inayokubalika na wazazi /walezi wake, hataruhusiwa kubadili dini/dhehebu akiwa shuleni isipokuwa kwa taarifa maalum ya mzazi/mlezi kwa uongozi wa shule endapo anampa uhuru mwanae kujichagulia kikundi cha kuabudia. Mawasiliano ya mahitaji mengine yoyote ya mwanafunzi vikundi au kikundi cha dini yatafanywa na kuwasilishwa kwa mzazi na makamu mkuu wa shule.

21. Wakati wa kurudi nyumbani kipindi cha likizo Mzazi/Mlezi atatakiwa kumfuata motto shuleni au atalipia nauli ya mwanae na gharama ya mlezi kutoka shuleni amsindikize nyumbani. Mtoto hatakabidhiwa kwa mtu amabaye uongozi haumtambui isipokuwa kwa maelekezo ya Mzazi/Mlezi.

## MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

Mwanafunzi anaweza kufukuzwa shule mara moja kama atachupa kwa makususdi mipaka ya uislamu kama vile;

1. Kutosimamisha swala (waislamu TU).
2. Wizi.
3. Uasherati, Ubakaji, Ushoga na ulawiti.
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya, biashara ya madawa yote ya kulevya.
5. Uvutaji bangi
6. Makosa ya jinai.
7. Kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzake, au mtumishi.
8. Kuharibu mali ya umma na ya watu wengine.
9. Kudharau Bendera ya Taifa. Picha za viongozi wa Taifa, Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
10. Kuoa au kuolewa, kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi.
11. Kupata mimba au kutoa mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
12. Kugoma, kuchochea au kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
13. Kukataa adhabu halali.
14. Kutofanya mitihani ya ndani na mazoezi.
15. Kutoroka shuleni.
16. Kumiliki simu ya mkononi ukiwa hapa shuleni
17. Kuingia kwenye vilabu vya pombe, nyumba za kulala wageni na katika kumbi za starehe.

## MAMBO MENGINE MUHIMU

Fomu za kujazwa na kurudishwa shuleni pamoja na fomu hii

1. Fomu ya taarifa muhimu za mwanafunzi na mzazi/mlezi.
2. Fomu ya ahadi ya mwanafunzi kuwa mtiifu na kutii sheria na kanuni zote za shule na kutoshiriki katika vitendo viovu kwa muda wote atakaokuwa shuleni. Hii ni pamoja na ahadi ya mzazi kukubaliana na kutekeleza maelekezo yote yaliyotolewa na shule.
3. Fomu ya mkataba maalumu kwa mwanafunzi kutomiliki simu awapo shuleni.
4. Fomu ya **Medical Examination:** Mwanafunzi apimwe, ijazwe na mganga, ipigwe muhuri na ikabidhiwe shuleni mara tu anaporipoti.

***Tunatazamia ushirikiano wako ili kuleta mafanikio Ahsante,***

**ABDULJALILU S. MUSTAPHA**
**MKURUGENZI WA SHULE**

RAUDHWA MODERN ISLAMIC SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 166,
NYAKANAZI - BIHARAMULO - KAGERA
RAUDHWA SCHOOLS
PHONE :+255789 588 152
+255758259520
+255715712238
EMAIL : raudhwaschools@gmail.com

Picha ya mwanafunzi ya hivi karibuni

## FOMU YA TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI

### A. TAARIFA ZA MWANAFUNZI:

(i) Jina kamili
…………………………………………………………………………………….………

***Andika majina uliyotumia katika mtihani wa kumaliza Kidato cha nne.***

(ii) Tarehe ya kuzaliwa ……………………………..… (**ambatanisha nakala ya cheti za kuzaliwa**).

(iii) Umri …………………………………………………… Jinsi ………………………

(iv) Mahali alipozaliwa:
Mkoa:………….……..…… Wilaya: ……………………… Kata/Mtaa ……………………………

(v) Mahali anapoishi:
Mkoa: ……………………….. Wilaya: ……………………… Kata/Mtaa …………………………

(vi) Taarifa za shule ambayo mwanafunzi alifanyia mtihani wa kuhitimu elimu ya sekondari (Kidato cha nne):
Jina la Shule: ...………………………… Halmashauri: ..… ……………… Mkoa: ……………..……

(vii) Mwaka ambao mwanafunzi alimaliza kidato cha nne: …………………………………………..…

(viii) Namba ya mtihani wa kidato cha nne ya mwanafunzi: ……………………………….…………

(ix) Ulemavu wa viungo. Kama anao eleza kwa maandishi aina ya ulemavu na vifaa anavyovitumia kumsaidia.
……………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………….
…………………………………………………………………………………………………….

(x) Taarifa ya afya ya mwanafunzi inatakiwa iwekwe wazi. Matatizo yote ya kudumu ya kiafya yanayomsumbua mwanafunzi yajulikane na hatua ambazo huchukuliwa kutatua matatizo hayo yanapompata pia zijulikane. Kwa wale wanafunzi watumiao dawa maalum pindi wauguapo, wanatakiwa kuja na dawa hizo na kuzikabidhi kwa viongozi wa shule.

### B. TAARIFA ZA MZAZI AU MLEZI:

1. Jina kamili ………………………………………………...…………………………….……
2. Anuani ya kudumu ……………………………….…………………………………………...
3. Namba ya simu: Nyumbani ……………………………… Ofisini ………………………….
4. Kijiji/Mtaa:…………………………..……Kata:…….…………..……………Tarafa:………..…
5. Wilaya:…………………………………..…..Mkoa:……………………………………………
6. Uraia………………………………...……….Kazi:……………….……………………………
7. Dini…………………………………..……Dhehebu:………………………….……………
8. Tafadhali eleza kama ni mzazi (Baba au mama) au mlezi ……………………….……………...

**RAUDHWA MODERN ISLAMIC SECONDARY SCHOOL**

P.O.BOX 166,
NYAKANAZI - BIHARAMULO - KAGERA
RAUDHWA SCHOOLS

PHONE : +255789 588 152
+255758259520
+255715712238
EMAIL : raudhwaschools@gmail.com

# FOMU YA AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi (**Jina Kamili la Mwanafunzi**) ……………………………………………………………………..….

Naahidi kuwa mtiifu na kutii sheria na kanuni zote za shule. Sitashiriki katika vitendo viovu kwa muda wote nitakaokuwa shuleni, mfano: migomo, fujo, makosa ya jinai, n.k.

Sahihi ………………………………..………… (mwanafunzi) Tarehe …….………………

**MZAZI / MLEZI (Ajaze Sehemu hii)**

(i) Mimi mzazi/mlezi wake nathibitisha kuwa mwanangu …………………..………………… amesoma na ameelewa kanuni na taratibu zote za shule.

(ii) Ninapenda ifahamike kuwa dini ya mwanangu ni ………………………….. dhehebu lake ni …………………………………

(iii) Ninaruhusu / Siruhusu mwanangu kushiriki katika makongamano au Warsha za Kidini nje ya shule. (**NB: Ikiwa ni lazima wanafunzi kushiriki shughuli hizo nje ya shule wapelekwa na viongozi wa shule na Mwalimu mlezi wa kikundi**).

(iv) Aidha, mimi ……………………….……………………………………. ambaye ni Mzazi/mlezi, nimesoma/nimesomewa kanuni na taratibu zote za shule na maagizo mengine ya shule yanayomhusu mwanafunzi ……………………………………………… na ninaahidi kutimiza wajibu wangu nikiwa Mzazi/Mlezi wa mtoto huyu kwa kumshauri ipasavyo pamoja na kumtimizia mahitaji yake ya shule kama nilivyoelekezwa kwenye fomu ya mahitaji ya mwanafunzi.

Jina La Mzazi/Mlezi: ………………………………………………………….……………………

Sahihi Ya Mzazi/Mlezi: ……….……… Na Simu ……………. Tarehe ……………

**TAARIFA NA MAWASILIANO YA WATU WA KARIBU NA MWANAFUNZI**

(Hawa watahusika kwa kumleta/ kumfuata mwanafunzi shule inapofungwa au inapofunguliwa)

(i) Jina: ……………………….……………………………………..….

Namba ya Simu: ………..………………………………………

Mahali anapoishi: ………………………………………………

PICHA YA HIVI KARIB BABA MZAZI

(ii) Jina: ……………………….………………………………………

Namba ya Simu: ………..………………………………………

Mahali anapoishi: ………………………………………………

PICHA YA HIVI KARIBUNI MAMA MZAZI

(iii) Jina: ……………………….…………………...…………………

Namba ya Simu: ………..………………………………………

Uhusiano: …………………………………….…………………

Mahali anapoishi: ……………………………………..…………

PICHA YA HIVI KARIBUNI MLEZI WA 1.

(iv) Jina: ……………………….……………………….………………

Namba ya Simu: ………..……………………….……………

Uhusiano: …………………….. ………………………………

Mahali anapoishi: ………………………………………..………

PICHA YA HIVI KARIBUNI MLEZI WA 2

P.O.BOX 166,
NYAKANAZI - BIHARAMULO - KAGERA
RAUDHWA SCHOOLS
PHONE :+255789 588 152
+255758259520
+255715712238
EMAIL : raudhwaschools@gmail.com

**HATI YA MAKUBALIANO KATI YA VIONGOZI WA SHULE, MWANAFUNZI PAMOJA NA MZAZI KUHUSU SHERIA YA KUTOMILIKI SIMU MWANAFUNZI AWAPO SHULENI**

---

Kutokana na sababu kuwa suala la wanafunzi wa Bweni kumiliki simu wawapo shuleni bado linaendelea kuathiri masomo ya wanafunzi, licha ya kukatazwa na sheria za shule, ikijumuishwa kwenye makosa yasiyo na marudio (yasiyosameheka), sheria No. 16. Imekubaliwa kuwa mwanafunzi yeyote atakayekutwa na simu ataondolewa shuleni na kusubiri maamuzi ya Bodi ya shule. Ambapo itapendekezwa na kamati ya nidhamu kuwa mwanafunzi huyo afutwe shule au atafutiwe shule nyingine na mzazi wake kulingana na mazingira ya kosa hilo.

Jina la Mwanafunzi: ………………………….. Sahihi: ………………..….. Tarehe: ……..………

Jina la Mzazi / Mlezi: ………………………….. Sahihi: ………………..….. Tarehe: ……..………

Jina la Mwl. wa Nidhamu: …………………….. Sahihi: ………………..….. Tarehe: ……..………

Jina la Mkuu wa Shule: ……………………… Sahihi: ………………..….. Tarehe: ……..………

**RAUDHWA MODERN ISLAMIC SECONDARY SCHOOL**

P.O.BOX 166,
NYAKANAZI - BIHARAMULO - KAGERA
RAUDHWA SCHOOLS

PHONE :+255789 588 152
+255758259520
+255715712238
EMAIL : raudhwaschools@gmail.com

Picha ya mwanafunzi ya hivi karibuni

*To: The Doctor concerned,*

**RE: MEDICAL EXAMINATION FORM**

**Please examine the following and furnish the School Management Team with his/her current health status.**

NAME: ………………………………………………………… Age: ……………….. Sex: ……………

ADDRESS: ……………………………………………………………………………………………

1. **GENERAL EXAMINATION**
   (a) Ears: ……………………………………………………………………………………
   (b) Eyes: …………………………………………………………………………………
   (c) Skin: ……………………………………………………………………………………
   (d) Upper & Lower extremities: ……………………………………………………………
   (e) Chest: …………………………………………………………………………………
   (f) Abdomen: ………………………………………………………………………………
   (g) Dental: …………………………………………………………………………………

2. **PAST MEDICAL HISTORY**

   ……………………………………………………………………………………………………

   **LABORATORY EXAMINATION**
   (a) Urinalysis: ……………………………………………………………………………
   (b) Stool:……………………………………………………………………………………
   (c) Sputum: ………………………………………………………………………………
   (d) B.S: ……………………………………………………………………………………
   (e) H.B: ……………………………………………………………………………………
   (f) Widal Test: ……………………………………………………………………………
   (g) Pregnancy Test: ………………………………………………………………………

Remarks:

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

Name: …………………………………………………Title: ………………….. Signature: …………

Date: ……………………………… Official Stamp

raudhwa
modern islamic schools
LIBERATION FOR THE NEW GENERATION